

SWAHILI FORUM 23 (2016): 47-63

USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA ZA KITHAKA WA MBERIA

GRACE NJERI WAWERU

Makala haya yanachunguza mtindo wa usimulizi katika tamthilia za Kithaka wa Mberia na kutoa ufanuzi wake. Tamthilia zenyewe ni *Natala* (1997), *Kifo Kisimani* (Death at the Well, 2001) na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (Flowers in the Morning Sun, 2004). Vipera vyta usimulizi vinavyochunguza ni methali, nyimbo/ngoma, sauti na hadithi. Usimulizi ni mbinu ya fasihi simulizi iliyo na jadi ndefu. Kutokana na msingi huu, wa Mberia alioanisha usimulizi na ujumbe wa tamthilia zake ana-powasawiri watusika wake kuitia matendo yao na mazungumzo yao jukwaani. Umuhimu wa matumizi ya mbinu ya usimulizi katika tamthilia teule unaonekana kupuuzwa na wahakiki wengi. Kwa hivyo, madhumuni ya makala haya ni kuangazia umuhimu wa usimulizi katika usawiri wa maudhui mbalimbali na kuthibitisha kuweko kwa matumizi ya usimulizi katika tamthilia teule. Ni makala ambayo yatawafaidi wanafunzi katika vyuo vinavyotoa masomo ya fasihi. Makala haya yanamdhiriwa wa Mberia kama mtunzi shupavu, anayeteka makini ya hadhira yake kwa kuiwezesha kutafakari zaidi kuhusu masuala anayojadilia tamthiliani, kwa matumizi ya usimulizi.

This paper analyses narrative style in Kithaka wa Mberia's plays. The plays analysed are *Natala* (1997), *Kifo Kisimani* (Death at the Well, 2001) na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (Flowers in the Morning Sun, 2004). The elements of narrative style analysed are proverbs, songs/dances, voice and epic. Narrative style has a long history in oral literature. It has been integrated into written literature and thus lost its initial outlook which had led to its disregard by many analysts in the past. The objectives of this essay are to discuss narrative style in the selected plays, and to show how it functions to create empathy on the part of the reader which helps her/him to internalise the themes conveyed. Furthermore, this essay intends to stimulate further research on narrative style in Swahili drama.

1. Utangulizi

Makala haya yanachunguza mbinu ya usimulizi katika tamthilia tatu *Natala* (1997), *Kifo Kisimani* (2001) na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (2004) zilizoandikwa na Kithaka wa Mberia. Chanzo cha matumizi ya usimulizi kimejikita katika fasihi simulizi, kwa hivyo mbinu hiyo husa-haulika na kupuuzwa sana katika uchanganuzi wa matini za fasihi andishi. Kwa mujibu wa Finnegan (1989: 5) na King'ei na Kisovoi (2005: 4) usimulizi ni mbinu kongwe ya kimtindo au matumizi ya lugha iliyoanza punde tu binadamu alipojua kuzungumza na mwenzake. Mbinu za kisimulizi zilirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo jamii zilipokusanya baada ya kazi za kutwa. Umahiri wa kuwa na kumbumbuku za kisimulizi ulihitajika kwa kiasi kikubwa ili kuhifadhi simulizi kadhaa kama vile hadithi na nyimbo ubongoni, kwani jambo ambalo halijaandikwa ni rahisi sana kusahaulika au kupotoshwa. Hii ina maana kuwa jamii zilihitajika kusimuliana mambo muhimu mara mara ili mambo hayo yaweze kukolea ubongoni.

GRACE NJERI WAWERU

Kulingana na Wamitila (2004: 13-17, 2008: 134) usimulizi ni mbinu ya fasihi simulizi, ambayo ni fasihi iliyokusudiwa kuwasilishwa kwa njia ya mdomo. Fasihi simulizi ni fasihi iliyo kongwe zaidi ikilinganishwa na fasihi andishi na iliyozuka kabla ya maandishi kuvumbuliwa. Hata hivyo fasihi simulizi imeathiriwa sana na fasihi andishi tangu kuvumbuliwa kwa uchapishaji. Tamthilia ni utanzu mmojawapo wa tanzu za fasihi andishi zinazoigiza matendo ya binadamu lakini huweza kutumia mbinu za fasihi simulizi. Kama anavyosema pia Wamitila (2002: 75) matumizi ya mbinu za fasihi simulizi katika tamthilia yalianza wakati wa enzi za akina Aristotle. Maigizo yaliimbwa au nyimbo zikatanguliza maonyesho. Athari za fasihi simulizi katika fasihi andishi bado zinajitokeza katika tamthilia hadi hivi leo. Aidha, mtunzi hutumia usimulizi kuunda mpatano wa kimaonyesho unaoingiliana na vipengele vingine kama msuko na wahusika katika usawiri wa maudhui.

Usimulizi unaweza kuainishwa katika makundi sita makuu: mazungumzo, maigizo, hadithi, ushairi, semi na ngomezi. Makala haya yanachunguza vipengele vinne vya usimulizi: methali, nyimbo/ngoma, sauti (zinaweza kupatikana katika makundi yote sita ya usimulizi) na hatimaye mighani (hadithi). Ngoma imechunguzwa pamoja na nyimbo kutokana na mwngiliano mkubwa wa vipera hivyo viwili.

Watafiti kadhaa wameishughulikia tamthilia ya Kiswahili katika kazi zao. Kwa mfano Mose (2005) amechunguza taashira za kifo katika tamthilia za *Mukwava wa Uhehe* (ya Mugyabuso Mulokozi), *Amezidi* (ya Said Ahmed Mohamed), *Kilio cha Haki* (ya Alamin Mazrui) na *Visiki* (ya Khaembra Ongeti). Ayodi (2011) ametafiti matumizi ya tashtiti katika tamthilia za *Mashetani* (ya Ebrahim Hussein), *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (tafsiri ya mchezo wa Nikolai Gogol), *Amezidi* (ya Said Ahmed Mohamed) na *Usaliti Mjini* (ya Francis Imbuga). Nkonge (2014) amelishughulikia suala la ujumi mweusi katika tamthilia za *Nitaolewa Nikipenda* (tafsiri ya mchezo wa Ngūgī wa Thiong'o) na *Mkwava wa Uhehe* (ya Mugyabuso Mulokozi). Hata hivyo, hakuna utafiti ambao umefanywa kuhusiana na usimulizi katika tamthilia za wa Mberia. Kwa hivyo makala haya yatasaidia katika kuliziba pengo la utafiti lililopo.

Makala haya yanaongozwa na nadharia ya usimulizi. Kwa mujibu wa Simpson (2004: 20) pamoja na Cobrey (2005: 1-5) nadharia ya usimulizi ina maana ya usomi unaohusiana na uchananganuzi wa usimulizi. Nadharia hii iliasisiwa kutokana na nadharia ya umuundo pamoja na urasimi wa Kirusi. Fabula na ‘syuzhet’/‘sujet’ ni istilahi zilizoasisiwa na wana urasimi wa Kirusi zinazohusishwa na nadharia ya usimulizi na huelezea muundo wa usimulizi. Mihimili ya nadharia hii ni miwili. Kwanza kuna ploti (*fabula*) ambayo ni mpangilio wa matukio yaani tukio moja baada ya jingine katika hadithi na huunda kitovu cha usimulizi. Pili, kuna usemi wa usimulizi (*syuzhet*) ambao huhusisha vipengele vya kimtindo kama vile matumizi ya methali, kisengere-nyuma na takriri. Katika makala haya, nadharia ya usimulizi inasaidia katika kuchanganulia

USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA ZA KITHAKA WA MBERIA

matumizi ya vipengele vya kimtindo: methali, sauti na nyimbo. Nadharia hii inasaidia pia katika kuonyesha mpangilio wa matukio muhimu ya hadithi ya Fumo Liyongo yanavyoona na mpangilio wa matukio ya tamthilia ya *Kifo Kisimani*.

2. Methali

Methali ni kipera kimojawapo cha fasihi simulizi kitumiwacho katika usimulizi ambacho huweza kuainishwa kama semi zenyе kauli fupifupi zilizojaa hekima. Kauli hizo huwa na maana wazi na maana batini au fiche ambayo ndiyo maana ambayo huzingatiwa. Methali za usimulizi huhusisha mahusiano ya moja kwa moja baina ya msimulizi na hadhira yake, tofauti na matumizi yake katika tamthilia ambamo mtunzi huziteua na kuziandika wakati wake ye ye mwenyewe na kumwachia msomaji kuzisoma wakati tofauti.

King'ei na Momanyi (2005: 35) na King'ei na Ndalu (2011: vii) wanasema kuwa methali ni msemo mfupi wa kimapokeo wenye busara usio wazi ambao una muundo mahsus. Ni utanze wa sanaa ya jadi unaotambulika kutokana na lugha na muundo wake. Methali haiwezi ikabuniwa na mtunzi na lengo lake huwa ni kuendeleza maadili ya jamii. Methali hutumiwa kwa ajili ya kufundisha, kuelimisha, kuonya, kuhukumu, kuusia na kuhamasisha. Uainishaji wa methali hutege-me a vigezo kadhaa. Kulingana na Wamitila (2004: 137-139) kuna vigezo saba vikuu ambavyo hutumiwa kuainisha methali:

- (1) Kigezo cha kiabjadi huainisha methali kufuatana na herufi zake za kwanza. Hiki ni kigezo ambacho hutumiwa sana katika vitabu kuainisha methali za jamii mbalimbali.
- (2) Kigezo cha kimaana hutumiwa kuchunguza maana za methali kwa kuzingatia tamathali zinazohusika.
- (3) Kigezo cha kisitiari hutumiwa kuainisha methali zilizo na muundo wa kisitiari (kitu kimoja huitwa kingine).
- (4) Kigezo cha kweli kinzani hutumiwa kuainisha methali ambazo zina sehemu mbili zinazokinzana kimaana.
- (5) Kigezo cha kiuamilifu hutumiwa kuainisha methali kulingana na utendakazi wake.
- (6) Kigezo cha kimuktadha huainisha methali kulingana na muktadha wake wa matumizi.
- (7) Kigezo cha kiishara huainisha methali kulingana na taswira za ishara zinazo-jitokeza.

Katika makala haya, kigezo cha kiabjadi kinatumika kama msingi wa kuziainisha methali zote zinazopatikana katika kila tamthilia na maana zake kutolewa kulingana na muktadha wa matumizi.

2.1. *Natala* (1997)

“Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu” (uk. 17). Hii ni methali ambayo inatumiwa na mhusika Bala akiwaambia “maiti” yaani abiria wa gari lililoja. Methali hii ni ya kutahadharisha na ina maana kuwa mtoto asiyefundishwa adabu na wazazi wake huerevushwa na dunia apatapo shida. Katika muktadha wa mchezo huu ina maana kuwa, licha ya kujua sheria za barabarani, “maiti” walipanda gari lililokuwa limejaa kupita kiasi (uk. 16) na baadaye wakajuta kwa kukumbana na mauti yao.

“*Hauchi hauchi unakucha*” (uk. 15). Mzee Balu anawaambia Natala na Bala methali hii. Hii ni methali iliyo na msisitizo – uwili wa sauti ambayo ni ya kuonya tusife moyo jambo linapoone-kana kana kwamba halifiki mwisho wake. Balu na Gane walikuwa wakidhania wangewasali siku iliyotangulia (uk. 16) lakini wamefika siku inayofuatia wakati wa jioni. Methali hii ni mwafaka katika muktadha huu kwani Bala na Natala wamekuwa wakisubiriwa kwa muda na hatimaye wamefaulu kuja na maiti.

“*Palipo na moshi hapakosi moto*” (uk. 3). Gane anamjulisha Natala kuwa Chifu angependa kuonana naye. Natala haelewi kwa nini Chifu anataka kuonana naye na anaanza kubishana na Gane. Inambidi Gane kumwambia methali hii ili kumkuliza. Methali hii ina maana kuwa, kila palipo na dalili ya kitu fulani, kitu hicho lazima kiwepo. Gane anataka Natala ajue kuwa Chifu lazima awe na ujumbe muhimu (moto) kwake ambao lazima aufikishe ye ye mwenyewe, kwani tayari amemtuma (moshi) kwake. Ujumbe wenyewe unatokea kuwa ni ‘Tango’ mumewe Natala aliyefariki (uk. 9).

“*Palipo na nia hapakosi njia*” (uk. 22). Bala anamwambia Natala methali hii ya kutia moyo inayomaanisha kuwa mtu anapokuwa na nia ya kufanya jambo fulani, hujitahidi kadri awezavyo kulitimiza. Katika muktadha huu methali hii ina maana kuwa Natala hawezikukosa pesa angalau kidogo za kumpa mhudumu wa Jengo la Ufuo (Bala) ili ampe mwili wa ‘bwanaye’, kwani anauhitaji. Hii inatuonyesha tamaa ya pesa walio nayo baadhi ya maafisa wa serikali ambao hawawajibiki kazini kwao.

2.2. *Kifo Kisimani* (2001)

“*Ahadi ni deni*” (uk. 101). Gege anamwambia Mweke methali hii inayotukumbusha kuwa tuahidi mambo ambayo tunajua tunaweza kuyatimiza. Mweke anaonekana kutoweza kutimiza aliomwahidi Gege (uk. 73). Gege amemuua Mwelusi (uk. 96) lakini hapewi Alida bintiye Mtemi Bokono kama alivyoahidiwa. Badala yake Batu anampa jina jipya ‘Mkuki wa Almasi’ na anaahidiwa ardhi kubwa.

“*Hasira hasara*” (uk. 39). Askari II anawaambia Askari I na Askari III methali hii ambayo hututahadharisha tusije tukafanya mambo kwa hasira lakini tuwe na makini na utulivu ili

USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA ZA KITHAKA WA MBERIA

tusijiletee balaa. Methali hii imetumika baada ya Andua kumletea Mwelusi chakula gerezani (uk. 36) na Askari III kuanza kukila. Askari I hafurahishwi na jambo hilo na anajaribu kukichukua kwa nguvu kutoka kwa Askari III bila mafanikio. Zogo linapozuka inambidi Askari II kuitumia methali hiyo ili kuwatahadharisha wenzake wasije wakajiingiza katika vita na kuumizana.

“*Bandu bandu huisha gogo*” (uk. 52). Methali hii ina maana kuwa vipande vidogovidogo vinaweza kuperasuliwa kutoka kwa kipande kikubwa cha mti, hadi mwishowe kipande hicho kikaisha. Kwa hivyo, tunaweza kufanikiwa katika kila jambo linaoonekana gumu kwetu ikiwa tutakuwa na subira na kuzidisha jitahada zetu. Azena anamtia rafikiye Tanya moyo kwa kumwambia methali hii ya kuhimiza. Tanya amekuwa akimpelekea Mwelusi chakula gerezani (uk. 51) lakini la kushangaza ni kwamba askari hawamruhusu kumwona mwanawe. Tanya amevunjika moyo na amtaka Andua mwenyewe apeleke chakula. Azena anamhimiza kwa methali hii kwani akijaribu tena na tena jitihada zake huenda zikafua dafu siku moja na akafanikiwa kumwona Mwelusi mwanawe.

“*Msiba huandamana na msiba mwenziwe*” (uk. 80). Tanya anamwambia Azena methali hii iliyio na maana kuwa jambo baya likitokea hufuatwa na jingine bayu. Azena amekuwa akimwambia Tanya kuhusu jamii jirani yao (Batuitui) ilivyotekeleza mashambulizi na watu kuuawa bali na mali kuharibiwa. Azena alipokuwa akitoroka aligongwa kwa jiwe. Isitoshe, mguu wake mmoja ulitegeka msuli alipokuwa akitoroka. Tanya anatumia methali hii kumliwaza Azena kwani ye ye ni rafikiye wa dhati na mara kwa mara, hufika kwake Tanya kumjulia hali (uk. 51).

“*Msiba wa kujitakia hauna kililio*” (uk. 44). Gege anajambia methali hii ya kutahadharisha iliyio na maana kuwa anayejingiza matatani hatakiwi kunung’ unika anapopatwa na shida. Tanya amekuwa akimhimiza Gege aende kumjulia hali nduguye Mwelusi lakini amekataa katakata na badala yake anajishughulisha na utengenezaji wa ala yake ya muziki ili wasichana wamtambue katika uwanja wa ngoma. Mwelusi nduguye amejiingiza katika harakati za kuikomboa Butangi (uk. 44-48); suala ambalo limemtumbukiza gerezani (uk. 21-34). Gege haelewi kwa nini Mwelusi ajiingize katika mambo ya hatari ndiyo maana anajambia methali hii ili angalau ajiliwaze.

2.3. *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (2004)

“*Asante ya punda ni mateke*” (uk. 7). Tungai anamsomea Kabitho barua kutoka kwa Watange iliyio na matumizi ya methali hii. Methali hii ina maana kuwa anayetendewa wema anaweza akatenda ubaya jambo ambalo si jema. Imeandikwa kwenye barua kuwa wageni (Wandiku) wote walioko Lolomo Kaskazini wahame kutoka mashamba ya Watange. Watange wadai kuwa wameishi na Wandiku kwa uvumilivu na kama majirani wema lakini Wandiku hawaonyeshi shukrani zozote kwo na hawana budi kuhama.

Methali hii hii imetumiwa tena na Toiche kwake Chebwe (uk. 64). Toiche anafika nyumbani kwa Chebwe na ameleta habari kuwa Nali bintiye amekamatwa na Wandiku (uk. 62). Yeye ametenda wema kwa kumletea Chebwe habari hizo nzuri ili achukue hatua yoyote muhimu kumwokoa bintiye. Hata hivyo Chebwe badala ya kutoa shukrani zake anapandwa na hamaki na kudai kuwa Toiche amemsaliti bintiye. Methali hiyo inatukumbusha kuwashukuru wanaotutendea mema.

“*Hakuna mrefu yasiyo na mwisho*” (uk. 1). Gachono anamwambia Nyagachi methali hii inayomaanisha kuwa kila kitu huwa na mwisho wake. Wanawake hao wawili ni wakimbizi walitomuliwa kutoka mashamba yao na Watange. Wanaishi katika vibanda vyta plastiki vilivyo na dhiki tele (uk. 2). Nyagachi anaonekana amekosa matumaini ya kutoka kwenye shida zinazowingira. Gachono hajafa moyo na anatumainia kuwa siku moja shida zao zitafika mwisho. Anatumia methali hiyo kumtia moyo Nyagachi rafikiye.

“*Lenye mwanzo halikosi mwisho*” (uk. 34). Kabitho anawaambia Nyagachi na Gachono methali hii iliyo na maana kuwa kila tukio liwe ni zuri au bayu hufikia hatima yake. Wanawake hao wawili wamemsimulia Tungai shida zao (k. 31-33) na analazimika kutumia methali hiyo ili kuwaliwaza na kuwapa matumaini mema; shida wanazopitia hazina mizizi, siku moja zitafika mwisho.

“*Mtoto wa nyoka ni nyoka*” (uk. 56). Kabitho anamwambia Tungai methali hii iliyo na maana kuwa mtu anaweza kuathirika kutohana na uzuri au ubaya wa wandani wake au wazazi wake. Katika muktadha huu, Kabitho anataka Watange wote wauawe. Kwa upande mwingine, Tungai anataka sheria za vita zizingatiwe (uk. 57). Mathalan, watu wasiohusika kwenye vita hawafai kushambuliwa. Kabitho naye aonelea kuwa mradi mtu ni Mtange (nyoka) afaa kushambuliwa – awaona Watange wote (nyoka) kama jamii moja iliyojaa maovu inayostahili kuangamizwa.

2.4. Kimalizio kuhusu uchanganuzi wa methali

Methali ni mbinu muhimu ya uwasilishaji wa ujumbe na muundo. Methali ambazo wa Mberia ametumia katika tamthilia zake zote tatu ni sahili, zinatumiwa kwa wingi, zinatumia maneno machachemachache na zinaoana vyema na muktadha wa matini. Kwa mkabala huo methali hizo zinasaidia katika kuweka ujumbe wa tamthilia wazi kwa njia ya kipekee ya usanii wa kisimulizi usiotatiza uelewekaji wa ujumbe wa tamthilia. Ni methali ambazo zinawapa wasomaji mazoezi ya kufikiri.

3. Uchanganuzi wa nyimbo

Kwa mujibu wa Kubo na wenzake (2011: 27) nyimbo ni tungo za kisimulizi zinazohusisha uteuzi na mpangilio maalum wa maneno yaliyo na mahadhi na hugawanyika katika beti. Uimbaji

USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA ZA KITHAKA WA MBERIA

huweza kuambatanishwa na uchezaji wa ala mbalimbali kama vile ngoma, kayamba na gitaa ili kuongezea ladha. Nyimbo zinaweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi. Nyimbo zimeenea sana mionganoni mwa jamii tofauti na huimbwa wakati wa shughuli mbalimbali. Kwa mfano kuna nyimbo za kazi, nyimbo za maombolezi, nyimbo za kumwongolea mwana, nyimbo za kuabudu na nyimbo za arusi. Hii ina maana kuwa nyimbo zinaweza kuainishwa kulingana na wakati zina-poimbwa. Nyimbo huimbwa ili kujichangamsha, kutoa mafunzo fulani, kubembeleza na hata kuburudisha. Njogu na Chimerah (2008: 172) wanasema kuwa “nyimbo na mashairi simulizi ndiyo yaliyokuwa *vitabu na magazeti ya wanajamii*” (msisitizo ni wangu). Wanachomaanisha wasomi hawa ni kuwa zilitoa mafunzo zikaenea sana na hata kupendwa na wengi. Ngoma nazo zimetumika kutoka jadi katika tamaduni za Waafrika katika sherehe kama vile za jando na unyago, arusi na katika kueneza ujumbe mbalimbali. Wakati mwangi ngoma huandamana na nyimbo.

3.1. *Natala* (1997)

Tamthilia inapoanza wimbo wa Natala akiwa sebuleni unasaidia kuyateka makini ya msomaji tayari kwa usomaji. Natala akiwa ndiye mhusika wa kwanza kuonekana jukwaani anaimba wimbo mtamu wa furaha wakati wa kazi; anapopiga pasi na kuchezeshachezesha mwili hadi Gane rafikiye anapoingia. Hata ingawa hatujapewa maneno ya wimbo huu, wimbo wake Natala umetumiwa na msanii kuteka makini ya hadhira yake. Aidha, wimbo huo unadhihirisha kuridhika kwa Natala katika maisha yake ya ndoa; ana mume anayempenda na kumtunza vyema. Anaweza kujikimu kimaisha na ndiyo maana tunaona mhusika kama Tila akija kwake kuombaomba (uk. 3) kwani anajua Natala hawezi kukosa bidhaa atakazo.

Tamthilia inapoelekea ukingoni mandhari yake ni nyumbani mwa Natala (uk. 41). Tango mumewe Natala aliyyedhaniwa kuwa tayari amefariki anarejea nyumbani (uk. 57). Hii ni furaha ilioye kwake Natala. Mwandishi anatuunganisha moja kwa moja kihisia na furaha hiyo anapotupeleka kwenye uchezaji wa ngoma unaoshirikisha wapenzi hao wawili pamoja na wahusika wenza (k. 60-61) ili kusherehekeea kurudi kwake Tango. Ni ngoma inayotoa mdundo unaoashiria hali ya furaha. Hata hivyo, wa Mberia hatuambii ni stadi yupi anayeshiriki katika upigaji wa ngoma hii. Kumtaja mpiga ngoma kungesaidia kuileta hadhira ya mwandishi karibu zaidi na tukio hili.

Uchezaji wa ngoma unatoa nafasi nzuri ya kuukaribisha wimbo wa Natala ambao ni mfupi, una mishororo minane na unatumia lugha ya mkato (uk. 61). Katika wimbo huu tunapata ufundi wa matumizi ya lugha. Kwanza tuna mbinu ya sitiari; Natala anatumia neno ‘zimwi’ kurejelea uchungu wa mateso ambayo amepitia kama mwanamke, kwa vile zimwi ni kiumba cha kutisha kinachodhaniwa kuishi msituni na kumdhuru mwanadamu. Pili, ni matumizi ya takririni neno ‘zimwi’ linaporudiwa mara mbili katika wimbo huu ili kutilia mkazo madhara ya mateso ya

GRACE NJERI WAWERU

Natala kama mwakilishi wa wanawake wengine. Tatu, wimbo huo unamalizia kwa swali la bala-gha Natala anapouliza, “Ni Natala wangapi ambao tayari wamo kinywani mwa zimwi?” (hapo hapo). Hilo ni swali la kuifikirisha hadhira kuhusu hali mbaya ambayo inaweza kuwa inawakumba wanawake wengine wengi ambao bado hawajui haki zao.

Wimbo wa Natala ni wimbo wa furaha kwani Tango mumewe amerejea, lakini hata hivyo umechanganyikana na masikitiko kwa wanawake wanaopitia dhiki na mateso kama yake Natala. Ujumbe wa wimbo huu ni muhtasari wa tamthilia nzima na unaoana vyema na wakati unapotokea (mwishoni mwa tamthilia). Natala anadokezea kuwa shida ambayo alikuwa nayo ya kunyanguanywa mali yake (uk. 53) baada ya kukataa kurithiwa na Wakene (uk. 40) haipo tena baada ya mumewe kurejea. Hapa tunatambua kuwa ugandamizaji wa mwanamke mahali popote pale ni tishio la ubinadamu mahali pengine popote pale. Natala ameweza kujikomboa kutoka kwa minyororo ya taasubi ya kiume. Natala anawazia akina mama wengine ambao wamo katika shida kama yake. Anawataka wao wenyewe wajikomboe jinsi alivyofanya. Anatumia wimbo ili kuwavutia wengine katika ujumbe wake. Je, wanawake wenzake wataweza pia kusimulia hatua ya ujasiri kama yake?

Natala anapomaliza kuimba wimbo wake uchezaji wa ngoma unaimarika (uk. 61). Ngoma hiyo inaiaga hadhira kwa njia ya kuridhisha kwani kwa ishara maalum ya mpigo wa ngoma, ina-katika wakati sawa na kuzima taa. Hii ina maana kuwa mpigaji wa ngoma ana umahiri wa kutosha wa uchezaji wa ala hii hivi kwamba hata ngoma inasema kwaheri. Ni ngoma inayoashiria tamati ya mchezo kwa kuiaga hadhira kwa njia ya burudani baada ya kushuhudia vituko na mikasa ajabu nyumbani kwao Natala na Tango. Aidha inatuliza nyoyo.

Alika na Bwanu wanaingia chumbani alimo mamao huku wakipiga makofi wakiimba wimbo wa watoto (uk. 24). Hata hivyo maneno ya wimbo huo hayajaandikwa pia. Wimbo huo wa watoto unanuiwa kutumiwa kama kitulizo na kututoa kwenye taswira nzito inayosababishwa na kifo. Ni wimbo ambao unanuiwa kumliwaza Natala na kumtoa kutoka dunia ya jitimai hadi ya uchangamfu.

Wakene anaingia nyumbani kwa Natala na kuanza kuimba wimbo wa mapenzi huku akichezesha mwili (uk. 11-12). Kwenye maneno ya wimbo, tunapata habari kuwa Natala anamuua Wakene kwa mapenzi kutokana na urembo wake na hata mabusu yake hivi kwamba ye (Wakene) anaungua na kuchemka rohoni. Wimbo huu umetumiwa kama kinaya katuonyesha jinsi Wakene ambaye ni mlevi (uk. 12) asivyowajibika katika ndoa yake. Natala ana mume anayempenda na hata inapodaiwa kuwa ameaga dunia anakataa katakata kurithiwa na Wakene. Wakene anapenda asikopendwa! Wimbo wenyewe una mishororo mifupimifupi iliyo na lugha ya mkato yenye ujumbe mzito. Umeja takriri ya maneno kwani “waniua ua” ni maneno yanayo-

USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA ZA KITHAKA WA MBERIA

rudiwa mara ishirini, katika wimbo ulio na idadi ya maneno 51. Urudiaji wa maneno hayo unatilia uzito wa mapenzi aliyo nayo Wakene kwa Natala.

Wimbo wa dini unatokea wakati wa mazishi ya ‘Tango’. Kasisi anaanzisha wimbo uitwao ‘Mungu Mpokee Mwanaao’ (uk. 29) ambaye ni Tango anayekisiwa kuwa amefariki. Maneno ya wimbo huu hayamo kitabuni. Watu wanatembea karibu na jeneza wakiwa kwenye mstari waki-imba wimbo huu. Wimbo huu wa maombolezi unaimbwaa pia wakati wa kuteremsha jeneza kaburini. Wimbo huu umetumika kuwafariji waliofiwa hasa mjane Natala; wajue kuwa ‘Tango’ amepokelewa mbinguni.

3.2. *Kifo Kisimani (2001)*

Kuna wimbo ulioandikwa wa “furaha” ambao ni wa kisiasa wa kumsifu Mtemi Bokono unaoimbwa na Tanya na Azena (uk. 81). Maudhui ya wimbo huo yametumiwa kwa kinaya kwani wahusika hawa hawaridhishwi na utawala wake Mtemi Bokono hata ingawa maneno yake ni ya kuusifia utawala wake. Umetumika kuukosoa ukasuku uliokuwepo kabla ya Wanabutangi kuzindukana. Ni mfano wa wimbo uendelezao propaganda na ukasumba uwazibao raia macho na masikio ambapo hawana nafasi ya kukashifu uongozi wa kidikteta. Hata hivyo, mambo sasa yamebadilika na baadhi ya Wanabutangi wameanza kuacha kumtukuza Mtemi Bokono kama Mungu wao ndiyo maana anapinduliwa (uk. 105). Kuwepo kwa maneno ya wimbo huo kunasaidia kuimarisha maudhui yanayoendelezwa ya utawala dhalimu. Wimbo wenyewe una mishororo mifupimifupi lakini mawazo mazito ya kisiasa. Aidha, wimbo huu unazo tamathali za semi kama vile tashbihi. Afya ya Mtemi Bokono inasemekana kuimarika na kulinganishwa na boriti la mkoko, boriti likiwa ni aina ya mti mrefu mnene unaotumiwa kujengea dari. Waimbaji wanajihimiza kwa kusema waimbe kwa furaha kwani wanailinganisha bahati yao ya kutawaliwa na Mtemi Bokono kuwa sawa na bahati ya mtende kuota jangwani. Mtende ni aina ya mti ambayo huota jangwani ingawa mazingira haya ni magumu.

Batu anapomwuliza Kaloo kuhusu mpangilio wa ngoma katika mkutano wa Mtemi Bokono (uk. 3) Kaloo anafurahia mada hiyo na papo hapo anaanza kucheza ngoma. Anamjulisha Batu kuwa viuno vitatingishwa mpaka viyeyuke. Ngoma kadhaa zingechezwa ikiwemo chakacha ambayo ni ngoma ya kitamaduni ya Waswahili wanaoishi mwambao wa pwani nchini Kenya na Tanzania, isipokuwa mkutano haufanyiki. Kaloo ndiye huongoza ngoma wakati wa sherehe. Inashangaza kuona kuwa kuna maandalizi kemkem ya uchezaji wa ngoma ya kisiasa ili kumtumbuiza na kumsifu Mtemi Bokono ilhali Wanabutangi huteseka si haba.

Askari II anapotupa macho nje ya gereza anauona umati wa watu ukielekea gerezani ukiimba wimbo (uk. 58). Wimbo unaoimbwa ni wimbo wa ukombozi lakini maneno ya wimbo huo haya-patikani tamthiliani. Umati unaelekea gerezani kumnasua Mwelusi kutoka mikono ya watesi

wake. Wimbo huo unawaleta wakombozi pamoja na kuwapa ujasiri wa kukabiliana na serikali dhalimu ya Mtemi Bokono.

3.3. *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (2004)

Kabitho anapowatembelea Gachono na Nyagachi kambini mwa wakimbizi, wanamjulisha kuwa wamekosa matumaini na lao sasa ni kumtegemea Mwenyezi Mungu. Baadaye Gachono ana-mwamrisha Kabitho aondoke ili wapate nafasi ya kuwa mbele ya Mungu. Anapoondoka wanaanza kuomba wakimlilia Mungu asikie na kuitikia kilio chao. Baadaye wanatilia maombi yao nguvu kwa kuimba wimbo wa imani (uk. 3). Wimbo huu ni wa dini ingawa maneno yake hayatambulishwi na mwandishi na unaonyesha kuwa wanamcha Mwenyezi Mungu. Wanatambua kuwa hali inaweza kuwa ngumu sana maishani kwani ‘dunia ni tambara bovu’. Wakati mwingine mateso hufika kwa wingi sana, lakini wanaomcha Maulana huweza kupata ushindi. Si ajabu kuwa mwishoni mwa tamthilia uhasama wa kikabila uliowaletea dhiki wanawake hao wawili unafikia kikomo.

Wimbo wa redio umeweza pia kutumika ingawa hatuyasomi maneno yake (uk. 4). Wimbo huo unaashiria kuanza kwa usomaji wa taarifa ya habari redioni. Wimbo huo unateka makini ya Kabitho anayejipanga na kuwa tayari katika usikilizaji wa habari hizo. Anapoisikiliza taarifa ya habari hiyo, anaanza kunung’unika papo hapo. Habari zinasema kwamba Mkuu wa Wilaya Bwana William Moche amewapongeza wakazi wa Lolomo kwa amani na utulivu ulioko. Kabitho adai kuwa habari hizo ni za uwongo mtupu! Kuna uwezekano kweli wa watu kuwa wametoroka mashamba yao yaliyomea magugu ilhali kuwe na amani na utulivu? Hii inaonyesha jinsi wata-wala wanavyoeneza uvumi kuititia vyombo vya habari unaosababisha kuuawa kwa Wandiku zaidi wanaporudi makwao (uk. 19).

Kuna wimbo wa vita unaoimbwa Toiche anapolifunza kundi la wapiganaji ingawa maneno ya wimbo huo hayomo tamthiliiani. Linapomaliza kufanya mazoezi ya viungo na kukariri kiapo, Toiche anamwamuru mwanafunzi mmoja aanzishe wimbo wa kivita na wenzake wanajiunga naye. Baada ya wimbo huo wanajipigia makofi kama ishara ya kuridhika (uk. 13). Wimbo huo unanuiwa kuwapa wapiganaji umoja na ujasiri katika makabiliano yao na adui. Ni wimbo unaoashiria kukosekana kwa amani na utulivu.

Chugu anamfuata rafikiye Waito hadi nyumbani kwao Nali. Nali anamwuliza kuhusu habari za chuoni na Chugu anamwambia kuwa bado wana “pambana na mlima” (masomo). Papo hapo Chugu anaanza kuimba wimbo wa furaha wa kuhimiza kutilia bidii masomo uitwao ‘Mlima Tutapanda, Mlima Tunapanda’ [*hivyo hivyo*]. Hatujapewa maneno zaidi ya wimbo huu unao-tumia lugha ya mkato na uradidi wa maneno. Nali na Waito wanajiunga na Chugu na wote watatu wanaimba na kucheza (uk. 46). Wimbo huu ulikuwa ukiimbwa katika chuo cha masomo na ni

USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA ZA KITHAKA WA MBERIA

wimbo wa kuwahimiza wanafunzi wafanye bidii katika masomo. Jitihada zinazohitajika masomoni ni sawa na jitihada zinazohitajika katika kupanda mlima.

Mwishoni mwa tamthilia makundi mawili hasimu yakiongozwa na Chebwe pamoja na Tungai yanaimbba nyimbo za kivita huku yakicheza ngoma (uk. 70). Nyimbo hizo ni za kuwatia moyo wapiganaji ili waweze kukabiliana vilivyo na maadui bila woga. Hata hivyo maneno ya nyimbo hizo hayamo tamthiliani. Kinaya ni kwamba Nali na Waito wanaingia katikati ya makundi hayo mawili na kuanza kuimba wimbo wa amani. Wimbo wa amani ni wimbo ulio na maneno ya kuleta umoja na uelewano. Wimbo huo unatuliza hali ya hatari iliyokuwa imeanza kuelekea hali ya usalama. Hali hiyo inatiliwa nguvu zaidi wacheza ngoma jukwaani wakiungana na Nali na Waito katika wimbo wao wa amani. Kilele cha mabadiliko hayo ni wakati ambapo Nali na Waito wanapofunga pingu za maisha. Wimbo wa arusi unaimbwaa huku Nali na Waito wakiondoka jukwaani. Nyimbo zinafanikiwa kuleta makundi mawili mahasimu ya Watange na Wandiku pamoja – damu ambayo ingemwagika inaokolewa.

3.4. Kimalizio kuhusu uchanganuzi wa nyimbo

Nyimbo zinasaidia katika kupambanua wahusika na maudhui kwa jumla. Ngoma zinapoambata-nishwa na nyimbo zinazua athari nzito zaidi ikilinganishwa na matumizi ya maneno ya kawaida. Ngoma zinasaidia kuendeleza utamaduni wa Mwfrika na kujenga taswira halisi ya matukio. Hata hivyo uhalisia na utamu wa nyimbo na ngoma kisimulizi haujitokezi vilivyo isipokuwa mwishoni mwa tamthilia ya *Natala*. Matumizi ya upigaji ngoma unaopishana taratibu na uwimbaaji wa Natala ulio na maneno halisi unazua utamu halisi wa nyimbo kwa kuzivuta hisia zetu zote kwenye hali hiyo na kutufanya tutamani kuwa mmojawapo wa tukio hilo. Ingekuwa vyema zaidi ikiwa wa Mberia angeefuata utaratibu huo katika sehemu nyingine za tamthilia hii ya *Natala* na sehemu zingine zote zilizo na matumizi ya nyimbo katika *Kifo Kisimani* na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi*. Muoanisho wa mbinu za matumizi ya lugha katika baadhi ya nyimbo unasaidia kuboresha matumizi ya nyimbo hizo kisanaa.

4. Sauti

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2014: 494) sauti ni “mlio unaotokana na mgongano wa vitu kama vile chuma, msuguano wa ala za kinywa au mwili wa kiumbe”. Sauti ya usimulizi inaweza kujitokeza katika vipengele vyote vya usimulizi kuititia sauti ya msimulizi halisi kama anavyoonekana machoni. Sauti katika tamthilia inahusisha maneno ya wazi yanayosemwa na wahusika. Maneno hayo husemwa hasa kutoka nyuma ya jukwaa. Sauti inaweza kuwa yenye ukali, upole, furaha, hasira, na kadhalika. Inaweza pia kupandishwa au kushushwa kulingana na ujumbe. Sauti inatuwezesha kung’amua mambo yaliyojisetiri akilini mwa mhusika na ambayo hawezi kukubali kuyatamka waziwazi mbele ya watu. Ujumbe muhimu huweza kuendelezwa

kupitia kwa matumizi ya sauti. Sauti inapotumiwa tamthiliani, ujumbe unaleta athari kubwa kwa hadhira lengwa. Na kama asemavyo Elbow sauti hutusaidia kumhisi mtunzi karibu nasi zaidi (ling. Elbow 1998: 423).

4.1. Uchanganuzi wa sauti katika *Kifo Kisimani* (2001)

Tamthilia inaanza kwa sauti inayofafanua mawazo ya Mwelusi kuhusu utawala wa Mtemi Bokono. Mandhari ni uwanja unaotarajiwa kufanyiwa mkutano wa umma (uk. 1). Sauti yenewe imejaa uchungu na ni kama muhtasari wa tamthilia nzima. Inatufanya tugundue awali ukatili wa Mtemi Bokono. Kutokana na sauti hiyo inatambulika kuwa kibanda ni kimoja kipekee cha kumsetiri Mtemi kutokana na jua, kwa sababu hana uwezo wa kulinyanya jua kama awatendeavyo Wanabutangi. Aidha, Mtemi Bokono ni mwenye uwezo mkubwa na anapenda kuwananyanya walio chini yake kwa kutumia askari wake. Hapo tunagundua mapema jinsi mitazamo ya Mwelusi na Mtemi Bokono isivyotangamana kamwe. Aidha, tunagundua pia kuwa maudhui ya tamthilia yenewe yanahusishwa na masuala ya kisiasa.

Kupitia kwa sauti ya ushawishi, Mweke anapenya akilini mwa Gege. Mojawapo ya sauti inamhimiza amwangamize Mwelusi ili apate fahari na mali. Sauti badala inamhimiza asithubutu kamwe kutenda unyama huo (uk. 74). Hilo linatuonyesha kuwa halikuwa jambo rahisi vile kwa Gege kufikia uamuzi wa kumwangamiza Mwelusi. Alipitia vita fulani na nafsi yake kabla ya kufanya uamuzi wake wa mwisho. Sauti hii pia inatilia mkazo nafasi ya Mweke kama kachero katili ambaye ni rahisi kumshawishi afanye kazi hii.

4.2. *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (2004)

Sauti ya kelele ya kuhuzunisha ya mtu mmoja, ya watu wengi nyuma ya jukwaa pamoja na kelele za watu wanaokimbizana zinasikika mara tu tamthilia inapoanza. Upembeni jukwaani kunasikika ukelele wa mwanamke (uk. 1). Sauti hizo zinatayarisha hadhira kushuhudia migongano ya aina fulani. Ni sauti zinazoashiria kutolewana baina ya wahusika kutokana na hali ya hatari inayowakibili. Ndiyo maana tamthilia yenewe inazungumzia mzozo wa kikabila ulio na msingi wake katika ugavi wa rasilmali – shamba.

Sauti ya vyombo vya habari inasikika redioni nyumbani mwake Kabitho ikimnukuu Mkuu wa Wilaya ya Lolomo Bwana Wiliam Moche (uk. 4). Sauti inayotumika ni ya kinaya kwa vile inawahakikishia wananchi wa Lolomo kuwa kuna amani na utulivu ilhali watu wametoroka ma-shamba yao kwa kuhofia usalama wao. Nyumba za watu zimechomwa na hata wengine wameuawa. Aidha, sauti hiyo inawadanganya baadhi ya wahusika kama vile Gachono anayerudi shambani mwake, na baadaye kutimuliwa na mumewe kuuawa (uk. 31). Hili linaonyesha kutowajibika kwa viongozi walio madarakani.

USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA ZA KITHAKA WA MBERIA

Sauti ya kutisha pia inasikika pale Toiche anapoelezea Chebwe kuhusu jinamizi lake la kutisha (uk. 26). Toiche anasema kuwa sauti isiyopendeza hisia inasikika na kumletea woga usio na kifani akiwa usingizini. Sauti hiyo inatoka kwa viumbe wa kushangaza. Tukio hilo linamwathiri Toiche mpaka anaghairi uamuvi wa kukifunza kikosi cha wapiganaji.

4.3. Kimalizio cha kuchanganua sauti

Sauti za usimulizi zinasaidia kuyateka makini ya msomaji na kumzamisha kwenye ujumbe. Sauti ya Mwelusi katika ufunguzi wa tamthilia ya *Kifo Kisimani* inatumika kuutambulisha mapema mgogoro unaopatikana tamthiliani. Inateka hisia zetu kwa njia ya kipekee na kutupa mshawasha wa kuisoma tamthilia. Sauti ya Mwelusi akilini mwa Gege inashiria hali ngumu ya mvutano wa nafsi ya Gege katika uamuvi wa mauaji ya nduguye Mwelusi. Sauti za usimulizi zinasikika kupitia wahusika mbalimbali na hata redioni. Sauti katika tamthilia ya *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* zinaonekana kuashiria hali ya hatari kwani maudhui yanayochukua nafasi kubwa katika tamthilia hii ni ya vita. Sauti ya redioni mbali na kuendeleza maudhui ya utawala dhalimu, inaendeleza pia athari za kizungu katika utamaduni wa Mwfrika. Sauti zote zinazotumika zinaoana vyema na ujumbe wa tamthilia na kusaidia kusukuma maudhui mbele. Ni sauti zinazopenya masikio ya msomaji na kusaidia kuuleta ulimwengu wa tamthilia karibu na ulimwengu halisia. Hata hivyo mbali na sauti hizi kuashiria maendeleo ya mbinu ya usimulizi, zinaififisha mbinu hii. Katika tamthilia ya *Natala* matumizi ya sauti dhahiri katika uwasilishaji wa ujumbe hayajitokezi.

5. Hadithi (mighani)

Utambaji wa hadithi jukwaani kwa njia ya usimulizi huwa na sifa tofauti na hadithi zinavyo-onekana katika tamthilia. Mambo kama vile sauti, miondoko, ishara na mihemko ya msimulizi hayajitokezi waziwazi katika uandishi wake. Hata hivyo, uandishi wa hadithi tamthiliani husaidia katika juhudi za kuiwasilisha tamthilia kwa wasomaji wake ingawa kwa upungufu fulani kwa sababu hadithi hukusudiwa kusimuliwa kwa njia ya mdomo.

Kwa mujibu wa Wamitila (2004: 39) tunaweza kuzigawa hadithi katika makundi mawili makuu. Kwanza, hadithi ambazo hujengwa kwa njia ya ubunifu na jamii fulani. Hizi ni hadithi za mapokeo za ubunifu. Jamii huhusika katika ubuni wa hadithi na hadithi hupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo. Baadhi ya mifano ni hekaya maarufu za Abunuwas, hurafa na hadithi za mazimwi. Pili, kuna hadithi ambazo zina misingi yake katika matukio ya kihistoria. Hizi huitwa hadithi za mapokeo za kihistoria. Kwa mfano, mighani, tarihi na visaasili.

Hadithi ya kipekee inayotambulikana katika tamthilia za wa Mberia ni ya aina ya mighani. Mighani ni aina ya hadithi ya kimapokeo ya kihistoria ambayo husimulia matukio ya kihistoria

ya majagina. Hata hivyo huweza kuchanganya na usimulizi wa kifasihi (yaani wa kibunifu) na kubadilisha ama kuficha ukweli wa historia.

5.1. Mighani katika *Kifo Kisimani* (2001)

Wamitila (2004: 84) ameweza kujadili kwa kina mighani inayosimulia maisha, wasifu na historia ya shujaa mmoja wa Uswhilini wa pwani ya Kenya aliyejulikana kama Fumo Liyongo (1160-1204). Baada ya kuyachunguza matukio muhimu ya mighani hiyo inabainika kuwa tamthilia ya *Kifo Kisimani* (2001) inasimulia mighani hiyo hiyo ya Fumo Liyongo yaani kuna mwingiliano wa mighani ile na tamthilia hii.

Fumo Liyongo aliiukia kuwa shujaa aliyepata umaarufu mkubwa katika jamii yake vile mfalme wa Pate akamwona kama tishio kwa ufalme wake akafanya njama ya kumwangamiza. Uadui baina ya Liyongo na mfalme ulimfanya kuhamia bara katika jamii ya Wasanye. Mfalme hakufa moyo akashirikiana na Wasanye kufanya njama ya kumkamata na kumwangamiza, lakini wakashindwa kwa sababu ya uwezo mkubwa wa Liyongo. Mwelusi naye anainuka katika jamii ya Butangi na Mtemi Bokono anamwona kama tisho kwa utawala wake na kutaka kumkomesha (uk. 11). Hatimaye mfalme aliwashauri Wasanye wamweleze Liyongo ahudhurie mchezo wa gungu (aina ya ngoma). Liyongo aliipenda sana ngoma hiyo akafunga safari ya kwenda mjini. Punde alipowasili alishikwa na jeshi kubwa la askari na kutiwa kizuizini. Tumeweza kumwona Mwelusi pia akishikwa na kufungwa gerezani (uk. 21).

Mamake Liyongo alikuwa akitayarisha chakula na kumpa kijakazi Saada ampelekee. Siku moja Liyongo alimtuma Saada kwa mamake kwa kumpa ujumbe ulioja mafumbo. Alimtaka amtayarishie mkate wa wishwa na aweke tupa ndani. Mamake alimtayarishia na alipopelekewa gerezani, alifanikiwa kuitumia tupa kuzikata pingu zilizomfunga pamoja na minyororo na akatoroka. Tukio hili ni sawa na la Atega anapompelekea Mwelusi mkate wa wishwa uliotiwa tupa ndani ambayo Mwelusi anatumia kujinasua kwa kuirereza minyororo iliyomfunga (k. 56-59; 62). Mfalme hakufa moyo akaendeleza njama yake ya kumuua Liyongo. Alishirikiana na mwanawe Liyongo aliyemfichulia siri kuwa babaye hangeweza kufa ila kwa sindano ya shaba. Mfalme alifurahishwa na mwanawe Liyongo akamwahidi kuwa angemwoza bintiye ikiwa angetekeleza kitendo cha kumuua babaye. Mwanawe Liyongo kusikia ahadi hiyo alimdunga babaye kitovuni akaaga dunia, lakini hakuozwa bintiye mfalme. Tukio hilo ni sawa na la Gege anapomdunga Mwelusi kisu tumboni na kuaga dunia (uk. 96), lakini haozwi bintiye Mtemi Bokono (Alida) kama alivyoahidiwa (uk. 101).

5.2. Kimalizio cha kuchanganua hadithi (mighani)

Mighani ya Fumo Liyongo ina msingi wake katika matukio ya kihistoria ya jamii ya Waswahili. Wa Mberia amefanikiwa katika kuichota, kuifinyanga na kubuni kisa kipyaa anachokisawiri katika

USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA ZA KITHAKA WA MBERIA

tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Hii ina maana kuwa tamthilia hii ni hifadhi bora la tukio la kihistoria kwani ushujaa wa mhusika mkuu Mwelusi unaingiliana kwa kiasi kikubwa na ushujaa wa Fumo Liyongo. Tamthilia za *Natala* na *Maua kwenye Jua la Asubuhi* hazionekani kuhifadhi muundo wa hadithi yoyote simulizi inayotambulikana.

6. Hitimisho na mapendelekezo

Nadharia ya usimulizi imesaidia katika kuchanganua mtindo wa usimulizi unaotumiwa katika tamthilia mbalimbali za Kithaka wa Mberia. Methali, nyimbo na sauti zinazodhihirika tamthiliani zimeainishwa na maelezo muhimu kutolewa kulingana na muktadha wa matumizi. Nadharia ya usimulizi imeweza pia kusaidia katika kulinganisha na kulinganua mpangilio wa matukio ya hadithi ya Fumo Liyongo na mpangilio wa matukio ya tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Mpangilio wa matukio haya mawili umeonekana kuingiliana kwa kiwango kikubwa na makala haya yanahitimisha kuwa wa Mberia amekopa mpangilio wa matukio ya hadithi ya Fumo Liyongo akaufinyanga na kuibuka na usanii mpya wa matukio katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*.

Makala haya yameweza kuweka bayana na kuendeleza umuhimu wa matumizi ya mbinu ya usimulizi katika uandishi wa tamthilia. Jambo hilo linasaidia katika uhifadhi wa mbinu hiyo kwa njia ya kipekee. Hii ni kwa sababu mbinu ya usimulizi inakusudiwa kusimuliwa kwa njia ya mdomo, kinyume na inavyojitokeza tamthiliani katika maandishi. Uandishi wa mbinu ya usimulizi hata ingawa umesaidia katika kutuhusisha nayo zaidi umetupunguzia mtagusano wa moja kwa moja unaonuiwa na fasihi hiyo iliyo kongwe zaidi. Hata hivyo wa Mberia amefanikiwa kwa kiwango fulani katika kuufufua usimulizi katika tamthilia zake. Amevichota baadhi ya vipera vya usimulizi na kuvioanisha na ujumbe andishi wa tamthilia zake kwa njia angavu isiyo na utata, jambo ambalo linaashiria kuimarika kwa matumizi ya mbinu hiyo. Walakini, kwa mtazamo wangu ingependeza kisimulizi na kiujumi angehusisha kipera cha nyimbo vyema zaidi kwa kuandika maneno halisi ya nyimbo zote katika tamthilia zote na kuziambatanisha na uchezaji wa ala kama vile ngoma vilivyo.

Matumizi ya usimulizi katika tamthilia zote tatu hayashabihiani kwa kiwango kikubwa. Kuna matumizi ya methali na nyimbo katika tamthilia zote tatu. Hata hivyo, matumizi ya sauti hayajitokezi katika *Natala* na matumizi ya hadithi hayajitokezi katika *Natala* na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi*. Kwa hivyo tamthilia ya *Kifo Kisimani* ndiyo inayoonekana kuongoza katika matumizi ya vipera vyote vinne vya usimulizi vilivyochunguzwa. Hii ndiyo tamthilia inayoni-vutia zaidi na imeweza hata kuteuliwa ili kutahiniwa katika mtihani wa kitaifa wa shule za upili nchini Kenya kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2012. Tamthilia ya *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* ndiyo inayofuatia kwa karibu kwa matumizi ya vipera vitatu na mwishowe ndiyo tunaikuta *Natala* inayotumia vipera viwili pekee. Ni dhahiri kuwa wingi wa matumizi ya vipera

GRACE NJERI WAWERU

vya usimulizi katika uandishi unaashiria kiwango cha ufundi wa kisanii wa hali ya juu unaoleta mvuto unaonata na kuiboresha kazi husika.

Kuchangiana kwa fasihi simulizi na fasihi andishi kunasaidia kuwa na fasihi mpya inayojitoshaleza kimalengo kwa kufaidiana na kukamilishana. Aidha, usimulizi una uwezo wa kuimariswa na kustawisha mbinu zetu za matumizi ya lugha katika usawiri wa maudhui. Kuathiriwa kwa fasihi andishi na usimulizi kumepelekea fasihi simulizi kupoteza sura na ladha yake asilia. Sura mpya ya fasihi simulizi imeweza kujitokeza katika maandishi na jina jipya la fasihi hii lafaa libuniwe. Kwa mfano, inaweza kuitwa fasihi ibuka au fasihi mseto. Vipera vya usimulizi vilivyo hakikiwa ni vinne pekee na kwa hivyo pana nafasi ya utafiti zaidi.

Marejeleo

Ayodi, Nancy Kahaviza. 2011. Tashtiti katika Tamthilia za *Mashetani, Mlaguzi Mkuu wa Serikali, Amezidi na Usaliti Mjini*. PhD Thesis, Chuo Kikuu cha Egerton.

Cobrey, Paul. 2005. Narratology. *The Johns Hopkins Guide to Literary Theory and Criticism*. Baltimore: John Hopkins University Press. <http://www.davidlavery.net/Courses/Narratology/websites_links_Readings.htm> (22/09/2016)

Elbow, Peter. 1998. *Everyone can Write: Essays Towards a Hopeful Theory of Writing*. New York et al.: Oxford University Press.

Finnegan, Ruth. 1989. *Oral Traditions and the Verbal Arts*. Edinburgh: Routledge.

Kin'gei, Kitula Geoffrey & Catherine Kisovoi. 2005. *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kin'gei, Kitula Geoffrey & Ahmed Ndalu. 2011. *Kamusi ya Methali*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Kubo Mary, Maria Mvati, Kiarie Kiongera & James Kanuri. 2011. *Mwangaza wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: National Educational Services.

Mberia, Kithaka. 1997. *Natala*. Nairobi: Marimba.

Mberia, Kithaka. 2001. *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba.

Mberia, Kithaka. 2004. *Maua Kwenye Jua la Asubuhi*. Nairobi: Marimba.

Mose, Ezra Nykundi. 2005. Taashira za Kifo katika Tamthilia za *Mukwava wa Uhehe, Amezidi, Kilio cha Haki na Visiki*. M.A. Thesis, Kenyatta University.

Njogu, Kimani & Rocha Chimerah. 2008. *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA ZA KITHAKA WA MBERIA

- Nkonge, Eliud. 2014. Ujumi mweusi katika tamthilia za *Nitaolewa Nikipenda na Mkwava wa Uhehe*. M.A. Thesis, Kenyatta University.
- Simpson, Paul. 2004. *Stylistics a Resource Book for Students*. Routledge: London.
- Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. 2014. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi et al.: Oxford University Press.
- Wamitila, Kyalo Wadi. 2002. *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix.
- Wamitila, Kyalo Wadi. 2004. *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus.
- Wamitila, Kyalo Wadi. 2008. *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.